



**JARAMOGI OGINGA ODINGA UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY  
SCHOOL OF EDUCATION, HUMANITIES AND SOCIAL SCIENCES.  
UNIVERSITY EXAMINATION FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF SPECIAL  
NEEDS EDUCATION- SPECIAL NEEDS EDUCATION  
2022/2023 ACADEMIC YEAR  
3<sup>RD</sup> YEAR 1<sup>ST</sup> SEMESTER  
MAIN CAMPUS REGULAR**

---

**COURSE CODE: ESB 3307**

**COURSE TITLE: BRAILLE II**

**EXAM VENUE:**

**STREAM: BED. SNE AND ECDE**

**DATE:**

**EXAM SESSION:**

**TIME: 2HRS**

---

**instructions**

- 1. Answer question 1 (compulsory) and any other 2 questions.**
- 2. Candidates are advised not to write on the question paper**
- 3. Candidates must hand in their answer booklets to the invigilator while in the examination room.**

## QUESTION ONE

**a) Andika maneno yafuatayo katika breli (10mks)**

- i. Bidii
- ii. Fedha
- iii. Chai
- iv. Debe
- v. Baada
- vi. Njaa
- vii. haja
- viii. Iba
- ix. Iga
- x. Ficha

**b) Andika herufi za abjadi za kiswahili katika breli (10mks)**

- a) A hadi J
- b) K hadi T
- c) U hadi Z

**c) Tunga sentensi ukitumia maneno kamili yanayosimamiwa na herufi za breli zifuatazo: (10mks)**

- i. Y
- ii. C
- iii. F
- iv. E
- v. P
- vi. J
- vii. K
- viii. M
- ix. I
- x. O

## QUESTION TWO

**Andika kwa nukta nundu zoezi lifuatalo:- (20mks)**

- a) Nukta nundu 1,2 na 4,5
- b) Nukta nundu 1,2 na 4
- c) Nukta nundu 1,2,3
- d) Nukta nundu 4,5,6
- e) nukta nundu 1,2.3 na 4,5
- f) Nukta nundu 1,3 na 4,6
- g) Nukta nundu 3 na 4
- h) Nukta nundu 1,2 na 4,5,6
- i) Nukta nundu 1,2 na 4,5,6
- j) Nukta nundu 1,2,3 na 4,5,6

### QUESTION THREE

**Andika sentensi zifuatazo kwa breli ukizingatia herufi zinazosimama badala ya neon: (20mks)**

- i. Wizara ya kilimo imetoa taarifa kuhusu mbegu mpya ya pilipili.
- ii. Asubuhi mimi hunywa chai kwa yai kabla ya kunywa dawa.
- iii. Neno hili limekuwa kama gogo kwenye roho.
- iv. Uwe na imani kwamba utapona homa.
- v. Jambo lako limetia fora katika eneo la ziwa viktoria.
- vi. Kuzuia ni bora kuliko kuponya.
- vii. Mawasiliano ni upashanaji habari kwa namna tofautitofauti.
- viii. Mwalimu ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii yote.
- ix. Jina lako limeandikwa katika Orodha ya wanaushirika
- x. Ni vyema kuelewa somo la nukta nundu.

### QUESTION FOUR

**Andika maneno haya ukitumia breli: (20mks)**

Waajiri wengi hupendekeza wanaoomba kazi watume maombi yao kwa kutumia baruapepe. Njia hii huondoa uwezekano wa wanaoomba kazi kutumia uofisadi ili wapate kazi. Aidha, njia hii husaidia kutunza mazingira kwani karatasi hazitumiwi. Katika elimu tarakilishi zinatumia shuleni kufundishia hivyo kurahisisha mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Aidha, kupitia tarakilishi iliyotandawizwa ama kuunganishwa kwa mtandao,

watu huweza kujuliana hali na kupashania habari mbalimbali kutoka pembe zote za dunia. Changamoto katika hatua hii ni ukosefu wa nguvu za umeme hasa mashambani. Aidha, gharama ya kununua tarakilishi ni kali mno hasa kwa mataifa yanayoendelea ikizingatiwa kuwa yana changamoto za kimsingi kama vile kutojua kusoma na kuandika, magonjwa na umaskini.

## **QUESTION FIVE**

**Andika maneno haya ukitumia breli: (20mks)**

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabuni. Hata hivyo, lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi. Fauka ya hayo, karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu kwenye lugha nyingine.

Inambidi mwanafunzi asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza. Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya mashairi na juu ya mahali mbalimbali ili kupata ujuzi wa mambo mengi.

Mawasiliano ni upashanaji habari kwa namna tofautitofauti. Njia za mawasiliano zimebadilika sana katika historia ya binadamu. Kwa mfano, zamani ingechukua siku nyingi kupitisha ujumbe baina ya watu wanaoishi sehemu mbalimbali. Siku hizi ujumbe hupitishwa katika sekunde chache katika masafa marefu.